

## 22D-Maddutw-Twabiy'iy - Maddul-Badal

### ii. مَدُّ الْبَدَل Maddul-Badal

Kanuni ya badal: ni kuja kwa hamzah mbili zenye kufuatana moja baada ya nyengine, ya kwanza ikawa na *i'raab* na ya pili ikawa saakin katika neno moja, hivyo hubadilishwa hamzah ya pili saakinah na kuwa herufi ya madd yenye kuwiana na *i'raab* ya hamzah ya kwanza.

Hukmu yake ni kuvutwa harakah mbili.<sup>1</sup>

Mfano jina la Aadam asili yake ni **ءَأَدَمَ** (A-dam); Hamzah mbili zenye kufuatana moja baada ya nyengine, ya kwanza ina *i'raab* ya fat-hah na ya pili ina sukuwn. Hamzah ya pili saakinah imebadilishwa na kuwa herufi ya madd yenye kuwiana na *i'raab* ya hamzah ya kwanza hivyo kusomwa: **آدَمَ**.

Mifano ifuatayo yote asili ya herufi ya madd katika mifano hii ni hamzah imebadilishwa na kuwa herufi ya madd yenye kuwiana na *i'raab* ya hamzah ya kwanza:

Mwanzo wa neno

ءَأَمِنُوا      إِيمَانًا      وَأَوْذُوا

Katikati ya neno

الْقُرَّانَ      مُتَّكِعِينَ      يَعُودُهُ

Mwisho wa neno

رءَا      وَبَاءُوا      ءَأَبَاءِي

---

<sup>1</sup> Hafsw 'an 'Aaswim *twariyq Ash-Shaatwibiyyah* huivuta harakah mbili. Ama riwaayah nyinginezo huvutwa zaidi ya harakah mbili, ndio maana Maulamaa wa fani hii wakaona kwamba hukmu hii ya مَدُّ الْبَدَل (maddul-badl) ihusiane na mlango huu wa مَدُّ الطَّبِيعِي (maddutw-twabiy'iy) badala ya mlango wa مَدُّ الْفَرْعِي (maddul-far-'iy)

